



TAARIFA KWA UMMA

**KUFUTWA KWA LESENI ZA UENDESHAJI BIASHARA YA MAFUTA YA
PETROLI KWA JUMLA**

Taarifa inatolewa kwa Makampuni yaliyoorodheshwa hapa chini kuwa, Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha kawaida cha 155 kilichoketi mnamo tarehe 27.08.2020 ilifuta leseni zao za uendeshaji biashara ya mafuta ya Petroli kwa jumla. Maamuzi hayo yalifikwa baada ya Bodi kujiridhisha kuwa Makampuni hayo yameshindwa kufanya biashara ya mafuta kwa jumla kwa mujibu wa kifungu cha 143(1) (a) cha Sheria ya Mafuta, Sura ya 392 na kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations) Rules, Toleo la Gazeti la Serikali Na. 380 la 2018.

Endapo kampuni haitaridhika na maamuzi hayo ya Bodi ya Wakurugenzi, inaweza kukata rufaa katika baraza la ushindani (Fair Competition Tribunal) kwa mujibu wa sheria ya EWURA, Sura ya 414 na Sheria ya Ushindani, Sura ya 285.

Makampuni ambayo EWURA imefuta leseni zao ni:

- Jina la Kampuni:** Alser Limited
Nambari ya Leseni: PWL-2017-001
Anwani ya Ofisi: Kiwanja Na. 7/8, Mtaa wa Ghana/ Ohio, Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam
- Jina la Kampuni:** Enoc Africa Limited
Nambari ya Leseni: PWL-2016-013
Anwani ya Ofisi: Kiwanja Na. 424, Toure Drive, Maeneo ya Oysterbay, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam
- Jina la Kampuni:** Express Oil Limited
Nambari ya Leseni: PWL-2016-015
Anwani ya Ofisi: Kiwanja Na. 66, Kitalu "F", Mtaa wa Kikale, Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam

4. **Jina la Kampuni:** Apex Energy Limited
Nambari ya Leseni: PWL-2016-010
Anwani ya Ofisi: Kiwanja Na. 14, Kitalu "C", Eneo la Tuangoma,
Wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam

Imetolewa na
Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA